## IKULU - DAR ES SALAAM

Wageni wachache walioalikwa Ikulu kushuhudia hafla fupi ya kumuapisha Mathew Mulumbi kama mkurugenzi mpya wa Shirika la UjasusiTanzania, waliwasili na kuchukua nafasi zao. Miongoni mwa wageni waliofika kushuhudia kiapo hicho ni marafiki wa karibu wa Mathew ambao ni  Papi Gosu Gosu na Ruby Rafael.

Hafla hiyo ya uapisho haikuwa ikirushwa mbashara kama ilivyozoeleka pindi viongozi wanapokula kiapo Ikulu. Hata uteuzi wa Mathew ulikuwa wa kimya kimya haukutangazwa bali walifahamishwa watu wachache wa muhimu kama viongozi wakuu serikalini na wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama.

Hatimaye Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliingia katika ukumbi mdogo ambao hafla ya uapisho ilifanyikia. Watu wote wakasimama. Wimbo wa taifa ukaimbwa. Bila kupoteza muda kiapo kikaanza. Mathew akaitwa. Akala kiapo mbele ya Rais kisha akaweka sahihi kiapo chake. Akapewa mkono wa pongezi na Rais.

Hakukuwa na hotuba yoyote iliyotolewa siku hiyo hivyo baada ya kiapo, likafuata zoezi la upigaji picha. Baada ya kukamilika, wageni wakatawanyika kwenda kuendelea na majukumu yao ya kila siku. Mathew Mulumbi akabaki Ikulu. Alikuwa na  mazungumzo ya faragha na Rais.

“Hongera sana Mkurugenzi na karibu sana Ikulu.” alisema Rais.

“Ahsante sana mheshimiwa Rais kwa imani yako kwangu. Hasa kwa kuniteua katika nafasi hii muhimu kabisa ya usalama wa nchi yetu.” Mathew alijibu. Wakatabasamu wote wawili.

“Ninakushukuru kwanza kwa kuipokea nafasi hii. Ungeweza kukataa uteuzi huu na hakuna adhabu yoyote ile iwapo ungekataa.” Rais Pius aliongeza kisha cheko likaibuka kati yao.

“Kukubali kwako kuitumikia nafasi nyeti kama hii ni heshima kwa niliyekuteua na kwa Watanzania ambao mimi niko hapa kwa niaba yao. Mathew, tambua ya kwamba umebeba majukumu mazito, hasa kwa wakati huu ambao nchi yetu iko katika vita kubwa ya kiuchumi” Rais alinyamaza kidogo

“Kama nchi tunapiga hatua kubwa kimaendeleo. Tunapambana kuelekea katika kujitegemea wenyewe kwa kutumia rasilimali zetu tulizo nazo lakini si safari nyepesi hata kidogo. Kupiga kwetu hatua ni jambo linalowaumiza sana mabeberu. Pamoja na mipango yao miovu dhidi yetu, nimeshaamua nchi hii itasonga mbele na tutakuwa nchi inayojitegemea kiuchumi. Hakuna taifa litakalotuyumbisha. Ili tuweze kushinda vita hii, tunahitaji sana kuliimarisha shirika letu la Ujasusi” alisema Rais na kunyamaza. Akainua glasi ya maji akapiga funda kadhaa kisha akaendelea.

“Kwa nini tunahitaji shirika imara la ujasusi? Akauliza na kumtazama Mathew kwa sekunde kadhaa halafu akaendelea

“Kama nilivyokwambia mabeberu hawafurahishwi na mbio zetu kuelekea kujitegemea hivyo hujuma ni nyingi. Tunavyozidi kupiga hatua kimaendeleo tunatengeneza pia maadui. Tunao

maadui wa nje na wa ndani pia. Kwa hapa ndani, wapo watanzania wasiopenda kuona nchi ikipiga hatua kimaendeleo. Wanazo sababu zao za kutaka hivyo. Wengine sababu za kisiasa, wengine kimaslahi nakadhalika. Hawa wamegeuka mawakala wa mabeberu. Siri za mipango yetu ya maendeleo zimekuwa zikiibwa na kupelekwa katika mataifa ya nje, lengo likiwa kutudhoofisha. Hawa ni Watanzania wachache wasaliti kwa nchi yao ambao wako tayari hata kuona nchi hii inaingia vitani ili wawafurahishe mabeberu. Nataka ulishughulikie hilo na tuwajue wasaliti wa taifa hili!" Alisema kwa ukali Rais Pius.

"Kutoka nje ya nchi, kuna mipango mingi ya kutudhoofisha inayofanywa na mataifa makubwa. Wameanza kuyatumia hata baadhi ya mataifa majirani zetu kutuhujumu. Kwa mfano, Tanzania hivi sasa tuna umeme wa uhakika, hii imepelekea tuwe na viwanda vingi vinavyozalisha bidhaa nyingi zenye ubora mkubwa na kwa gharama nafuu. Kwa hakika, hili halijawapendeza mataifa makubwa hivyo basi yametolewa maelekezo kwa baadhi ya mataifa yanayotuzunguka kuweka kodi kubwa katika bidhaa zote zinazotoka Tanzania kwa lengo moja tu la kuhakikisha bidhaa zetu haziingii katika masoko yao. Nchi hizo zinazofanya hayo zinapewa misaada mikubwa kutoka kwa mabeberu. Mathew hii ni vita lazima tupambane kuhakikisha uchumi wetu unakua kwa gharama zozote" Rais akanyamaza tena kidogo na kusukumia na funda la maji yaliyokuwa mezani.

"Mathew, kwa maelezo hayo machache naamini umeelewa ni kwa nini ninataka kuliimarisha shirika letu la ujasusi. Nataka

majasusi wetu wapenye na kuzidaka mbinu chafu za mabeberu dhidi yetu. Nataka wadake mbinu na mipango yote ya wapinzani wetu kibiashara. Nataka makuwadi wote wa mabeberu walioko hapa nchini wafahamike na wawekwe katika uangalizi mkali wa karibu bila wao kufahamu. Nataka wakipanga mpango usiku wa leo, kesho asubuhi tuwe na taarifa za walichokipanga kukifanya. ” alisema Rais Pius.

“Mheshimiwa Rais, hayo yote uliyonieleza ninayafahamu na ninakuahidi kuyashughulikia. Matokeo yake utayaona kinagaubaga. Sitakuangusha mheshimiwa Rais.” alisema Mathew.

“Ahsante sana. Tukiacha hayo, kuna suala lingine ambalo nataka nikueleze ulishughulikie kwa uzito mkubwa lakini kimya kimya bila watu kufahamu” Rais alinyamza kidogo halafu akaendelea.

“Wiki moja iliyopita, waziri wetu wa Mambo ya Nje Dr. Magnus Kalebi aliuawa akiwa nje ya nyumba yake akisubiri kufunguliwa geti. Alikuwa anatokea nchini Rwanda ambako nilimtuma kwa kazi maalum lakini kabla hajaniletea taarifa ya kile nilichomtuma, akauawa na mkoba wake wenye taarifa zote ukachukuliwa. Nina kila sababu ya kuamini kuwa mauaji yale ya waziri Magnus yana mkono wake kutoka nje ya nchi. Nitakueleza kwa nini ninaamini hivyo.” Rais akanyamaza tena kidogo. Uso wake ukaonekana kuingiwa na huzuni. Dhahiri mauji ya Dr. Magnus yalimkwaza.

“Kuna mazungumzo ya siri yanaendelea hivi sasa kati yangu na marais wa Rwanda na Burundi. Tunazungumza

namna ya kuziunganisha nchi hizi tatu kuwa nchi moja” Rais akanyamaza kidogo baada ya mshangao kuonekana usoni kwa Mathew.

“Sijakuelewa Mheshimiwa Rais.” alisema Mathew.

“Kuna mazungumzo ya siri yanaendelea hivi sasa kati yangu na marais wa Rwanda na Burundi ili kujaribu kuziunganisha nchi hizi tatu iwe nchi moja.” Rais akarudia kauli yake ile ile kisha akamtazama Mathew ambaye ni wazi alionesha kuhitaji maelezo zaidi.